OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA

HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

MAPENDEKEZO YA VIPAUMBELE VYA HALMASHAURI VITAKAVYOZINGATIWA KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
P. O. BOX 108.
Iringa

SIMU: +255 26 27025/2702828
Fax: +255 26 2702396/2701776
Email: ded@ iringadc.go.tz

APRIL 2017

1.0 **UTANGULIZI**

Katika kubaini Vipaumbele vya Halmashauri ya wilaya ya Iringa, mambo mbalimbali huzingatiwa ili kuwianisha hali halisi ya mahitaji ya jamii ya watu wa Iringa na uhalisia wa mambo ulivyo Kiuchumi, kijamii na kisiasa. Katika kuyachambua masuala mbalimbali, jumla ya maeneo Tisa (9) ya vipaumbele yamekubaliwa kuwa ni vipaumbele vya Halmashauri kwa sasa na kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) na Mpango Mkakati wa Halmashauri wa mwaka 2016/17 – 20120/21 vinavyobeba masuala (issues) yatakayohitaji kushughulikiwa kupitia Mpango na Bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa 2017/18.

Vipaumbele muhimu vya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kwa mwaka 2017/18 kama ilivyokuwa mwaka 2016/17 vimebainishwa kuwa ni Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri ambacho kinaendelea kuwa ni kipaumbele kikubwa cha kwanza (1). Kutokana na jukumu la kisheria la Halmashauri (mandatory obligation) la kutoa huduma bora na zinazotosha (quality and adequate services) kwa wananchi wake uwepo wa fedha za kutosha ni jambo la lazima. Hadi mwaka 2009/10 Halmashauri ya wilaya ya Iringa imekuwa ikitegemea fedha za nje (external funding) kwa 96% hali ambayo ni ya hatari kwa Halmashauri. Hii ina maana kuwa Halmashauri ilikuwa na uwezo wa kujitegemea wa 4% tu. Kwa bahati nzuri kwa mujibu wa mkaguzi mkazi wa mkoa wa Iringa Halmashauri imeongeza mchango wake katika bajeti yake ya mwaka kwa 12% kwa mujibu wa mahesabu wa mwaka 2013/14. Mageuzi ya makusudi ni lazima yaendelee kufanywa ili Halmashauri ijitegemee kwa mapato yake ya ndani na kupunguza utegemezi wa fedha za Serikali kuu, wafadhili na wadau wengine wa maendeleo kwa kiwango kilichopo sasa.

Elimu inakuwa ni hitaji kubwa la 2 la Halmashauri kutokana na Changamoto zinazoikabili sekta hii kwa sasa. Kilimo na Mifugo ni kipaumbele cha 3 cha Halmashauri kutokana na nafasi na uhusiano wa kimaisha iliyo nayo Sekta hii kwa wananchi wa Wilaya ya Iringa. Maji ni kipaumbele cha 4 ambacho kutopatikana kwake kunadumaza hata uwekezaji wa miradi mingine ya maendeleo mfano miradi inayohusisha ujenzi wa miundombinu, n. k. Aidha umuhimu wa maji unawafanya wananchi wautumie muda wao mwingi kuyatafuta na hivyo kuathiri shughuli za uzalishaji mali. Mapambano dhidi ya Ukimwi ni kipaumbele cha 5 kutokana na uzito na ukubwa wa athari zinazosababishwa na janga hili katika Halmashauri yetu. Ukweli ni kuwa juhudi zote za maendeleo na raslimali inayotumiwa na Halmashauri mwishoni hazitakuwa na maana kama walengwa wa maendeleo haya watakwisha kwa Ukimwi! Afya ni kipaumbele cha 6 cha Halmashauri kwa kuwa afya ya mtu ni mtaji wa kumwezesha kushiriki na kuhimili mikikimikiki ya kimaisha bila shida kubwa. Hifadhi ya Mazingira ni kipaumbele cha 7 kutokana na mchango wa sekta hii katika maendeleo ya sekta nyingine kama maji, kilimo (umwagiliaji maji ya mto Ruaha), mifugo, n. k. Kutokana na uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na Halmashauri katika miundombinu ya umwagiliaji (kutokana na mto Ruaha), suala la Hifadhi ya mazingira haliwezi kupuuzwa kwa vyo vyote! Barabara ni kipaumbe cha 8 kutokana na kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ni kubwa, na kuwa mawasiliano muhimu yanayotegemewa na wananchi ni barabara. Mtandao mzuri wa barabara utawezesha maeneo yote ya Halmashauri kufikiwa na mazao ya wakulima kuyafikia Masoko ya walaji wa bidhaa za kilimo na viwanda. Utawala Bora ni kipaumbele cha 9 cha Halmashauri kutokana na kuwa eneo hili ndilo injini ya kuratibu na kujumuisha vipaumbele vyote vilivyotambuliwa na Halmashauri. Kwa ujumla ikitazamwa kwa kina, vipaumbele hivi vinahusiana na kutegemeana kiasi kuwa si rahisi sana kuamua ni kipi hasa kipaumbele cha kwanza; cha pili, cha tatu, n. k. Katika sehemu ya 2.0 ya mapendekezo haya ya vipaumbele vya Halmashauri kila kipaumbele, zimeonyeshwa sababu za Kipaumbele husika kuwa katika nafasi hiyo kwa mtazamo wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kwa mwaka 2016/17.

2.0 UFAFANUZI NA SABABU ZA VIPAUMBELE VINAVYOPENDEKEZWA KUWA KATIKA NAFASI VILIVYOPO

NA	SEKTA	AINA YA VIPAUMBELE NA SABABU ZA KUWA VIPAUMBELE	VIPAUMBELE NA GHARAMA
1	**FEDHA**	**UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI** • Mapato ya ndani ya kutosha ya Halmashauri ndiyo yataiwezesha kumudu	- Kuendelea kuimarisha Kikosi kazi (Task Force) ili kukiwezesha kubaini vyanzo vipya vya mapato ya Halmashauri, kufuatilia na kushauri

		kikamilifu majukumu yake ya kutoa huduma bora za Kijamii na Kiuchumi kwa wananchi wake na hivyo kuhalalisha uwepo wake (confirm justification for its existence). • Halmashauri ya Wilaya ni wakala wa Serikali kuu iliyo na jukumu la kuhakikisha kuwa mali na maisha ya wananchi yanakuwa salama daima. Jukumu hili linahitaji raslimali fedha na watu walio na ujuzi unaofaa kuyasimamia majukumu haya. • Kama ilivyoelezwa katika utangulizi hapo juu, Mahitaji ya wananchi ni mengi na makubwa kuliko uwezo wa kifedha wa Halmashauri. Hivyo ni lazima juhudi za kutosha za kukusanya na kutumia raslimali fedha ziwepo kwa mujibu wa taratibu na sheria za Fedha zilizopo.	vizuri jinsi ya kuongeza Mapato ya ndani ya Halmashauri kupitia vikao 6 @ 250,000 = 1,500,000/=; ziara 6 za kufuatilia ukusanyaji @ 980,000 = 5,880,000 katika mwaka 2017/18. - Kuimarisha Idara ya Fedha sehemu ya Uhasibu wa Mapato kufuatilia, na kupitia mikataba ya wakala wa ukusanyaji wa mapato mbalimbali ya Halmashauri walau mara 6 kwa mwaka @ 350,000 = 2,100,000. - Kuchangia kwa fedha za ndani uwekezaji katika miradi ya kiuchumi ya Halmashauri kwa kutumia 35% (au 40%) ya jumla ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa mwaka 2017/18. - Jumla ya gharama za Sekta ya Fedha (Makusanyo ya ndani) **Tshs. 9,480,000/=**
2	**ELIMU**	**a) Shule za Msingi:** • Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi 148 wilayani. - Kuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za walimu katika shule za msingi. - Upungufu wa madawati na samani za shule za msingi. - Upo upungufu mkubwa wa madarasa ya awali katika shule za msingi. - Kuna upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi. - Ukamilishwaji wa majengo ya shule, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upatikanaji wa walimu wa kutosha ni masuala yanayosisitizwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM **b) Shule za Sekondari:** • Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za sekondari 28 wilayani. - Kuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za walimu katika shule za sekondari. - Upo upungufu mkubwa wa madarasa	**a) Shule za msingi:** - Ujenzi wa vyumba vya madarasa 10 na ukarabati wa madarasa 20 katika shule za msingi wilayani kwa gharama tya Tshs 240,000,000/= - Ujenzi wa nyumba 6 za walimu katika shule za msingi wilayani kwa gharama ya TShs 240.000,000/= - Ujenzi wa matundu 120 katika shule za msingi wilayani kwa gharama ya Tshs 50,000,000 - Ujenzi wa ofisi 10 za walimu na ukarabati wa ofisi 10 za walimu katika shule za msingi wilayani kwa gharama ya Tshs 150,000,000 - Utengenezaji wa samani za shule (Meza na viti vya walimu 30 na madawati ya wanafunzi 450) kwa gharama ya Tshs 45,100,000/= - Kuwezesha mafunzo kazini kwa walimu 600 juu mitaala mipya ya kufundishia kwa gharama ya Tshs 300,000,000/= **Jumla Shule za Msingi – Tshs.1,025,100,000/=** **b) Shule za Sekondari:** - Kukamirisha ujenzi wa maabara 10 na ujenzi na ujenzi wa maabara mpya 6 katika shule za sekondari kwa gharama ya Tshs 260,000,000/= - Kukamilisha ujenzi wa hosteli 2 na ujenzi wa hosteli 1 katika shule za sekondari 3 wilayani kwa gharama ya Tshs 510,000,000/= - Ujenzi wa nyumba 3 za walimu wa shule za sekondari @ 60,000,000 = Tshs. 180,000,000/=

		katika shule za sekondari. - Pamoja na juhudi kubwa za ujenzi wa maabara, bado upo upungufu wa miundombinu hii katika shule zetu za sekondari zilizopo, nyingi zikiwa hazijakamilisha ujenzi wa maabara ya 3. - Kuna upungufu wa madawati katika shule za sekondari - Kuna upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za sekondari - Uhaba wa mabweni ya kulala wanafunzi katika shule za sekondari. - Kuna Uhaba mkubwa wa walimu shule za sekondari. - Ukamilishwaji wa majengo ya shule, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upatikanaji wa walimu wa kutosha ni masuala yanayosisitizwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM.	- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 20 katika shule za sekondari Tshs. 400,000,000/= - Utengenezaji wa samani za maabara 10 mpya zilizokamilika kujengwa mwaka 2016/17 katika shule 10 za sekondari @ 20,000,000 = Tshs. 200,000,000/=. - Utengenezaji wa madawati 2,000 kwa ajili ya shule za sekondari Tshs 156,000,000/= - Utengenezaji wa meza 432 za walimu shule za sekondari kwa gharama ya **Tshs.** 15,000,000/=. - Ujenzi wa vyoo matundu 350 kwa gharama ya Tshs 175,000,000/= - Utoaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika shule za sekondari – Tshs. 40,000,000**.** - Ununuzi wa vifaa vya maabara na madawa kwa ajili ya shule 25 za sekondari kwa gharama ya Tshs.250,000,000/= **Jumla: Shule za Sekondari –Tshs. 2,186,000,000/=**
3	**KILIMO NA MIFUGO**	• Kuinua kipato cha wananchi, kuongeza ajira na kupunguza umaskini kupitia shughuli za kilimo na mifugo - Kuwa na uhakika wa chakula muda wote wa mwaka kwa kila kaya kwa kuhamisisha kilimo cha mazao ya muda mfupi na yanayostahimili ukame. - Matumizi ya zana bora, pembejeo za kilimo hususan, mbolea, mbegu bora na madawa ya kudhibiti visumbufu na kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika - Kuna fursa kubwa ya kilimo cha umwagiliaji katika wilaya kutokana na uwekezaji katika ujenzi wa skimu za umwagiliaji kwa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia kila chanzo cha maji kinachowezekana (mito, mabwawa, visima na maji ya mvua).	- Ujenzi na ukarabati wa miundo mbinu ya umwagiliaji katika kata za Mseke, Ilolompya, Itunundu, Mahuninga, Mgama, Luhota, Nduli, Nyangoro na Idodi – **Tshs. 2,400,000,000/=** - Uendelezaji na ufuatiliaji wa mazao mapya yaliyoanzishwa ya mikorosho, miembe na migomba – **Tshs. 14,000,000/=.** - Uzalishaji wa mboga mboga na matunda katika kata za Maboga, Idodi, Mgama, Mlowa na Lyamgungwe – **Tshs. 150,000,000/=** - Uzalishaji wa mbegu za kuazimia ubora kwa mazao ya Chakula kama mahindi na mpunga; na mazao ya Biashara kama tumbaku, alizeti, nyanya na vitunguu – **Tshs. 20,000,000/=.** - Ununuzi wa nyenzo za kufanyia kazi – pikipiki 10 @ 6,000,000 – **Tshs. 60,000,000;** gum boots 20 pairs @ 10,000 – **Tshs. 200,000/=;** makoti ya mvua 20 pairs @ 8,000 – **Tshs. 160,000/=.** - Ujenzi wa malambo 14 ya kuvunia maji ya kunyweshea mifugo katika kata za Nduli, Malengamakali, Izazi, Kihorogota, Migoli, Ilolo mpya, Itunundu na Mlowa @ 50,000,000 – **Tshs. 700,000,000/=.** - Ujenzi wa majosho 10 ya mifugo @ 100,000,000 katika kata za Nduli, Kihorogota, Itunundu, Mgama, Wasa, Nzihi, Idodi na

			Ifunda – **Tshs. 1,000,000,000.** - Kuandaa na kuendesha mafunzo kwa vikundi vya wakulima 270 – shamba darasa juu ya kanuni bora za kilimo na ufugaji @ 340,000 – **Tshs. 91,800,000/=.** - Kuandaa na kuendesha mafunzo ya kujenga uwezo kwa Wataalamu wa kilimo na mifugo 40 - **Tshs. 24,000,000/=.** - Kuandaa na kutoa huduma ya kuboresha afya ya mifugo (chanjo) kama ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na mbwa **- Tshs. 40,000,000/=.** - Kuandaa na kuendesha mashindano ya wakulima ya Nane nane katika vijiji, kata na wilaya na Kikanda jijini Mbeya – **Tshs. 40,000,000/=.** - Kuimarisha Vyama vya Akiba na mikopo, vikundi vya uzalishaji mazao na Masoko – **Tshs. 32,000,000/=** **Jumla - Kilimo/Mifugo – Tshs. 4,572,160,000/=**
4	**MAJI**	• Kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi, salama na ya uhakika kwa umbali usiozidi mita 400 kutoka kila kaya kutoka 69.2% hadi 72% - Kukamilisha miradi inayoendelea kujengwa. - Kukarabati miradi ambayo haifanyi kazi vizuri. - Upanuzi wa miradi iliyopo na kujenga miradi mipya. - Kutokuwepo kwa huduma ya maji kunawafanya wananchi na hasa akina mama kutumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya kazi za uzalishaji mali kwa ajili ya kaya zao. - Kuongezeka kwa mahitaji ya maji kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu. - Kuwepo kwa ugomvi kati ya wakulima na wafugaji kutokana na kunyang'anyana maeneo ya malisho na kilimo. - Maji ni hitaji namba 2 (baada ya hewa) kwa umuhimu kwa binadamu	- Ujenzi wa mradi wa maji kwa ajili ya vijiji vyote 12 vya kata za Nyang'oro na Kihorogota – Tshs. 2,670,000,000/=. - Kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji cha Malinzanga Tsh. 1,000,000 - Ujenzi wa mradi wa maji Izazi – Mnadani kwa gharama ya Tshs 725,056,271/= - Ujenzi wa mradi wa maji Migoli kwa gharama ya Tshs 1,385,930,662 - Ujenzi wa matanki na visima vya kuvunia maji ya mvua katika vijiji 33 vya tarafa ya Ismani – Tshs. 2,000,000,000/=. - Utafiti na ujenzi wa mradi wa maji wa Kinywang'anga hadi kijiji cha Mawindi na Ikengeza – Tshs. 780,000,000/=. - Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji katika jumuiya za watumia maji za Tanangozi – Ibangamoyo (Kalenga), Pawaga na Mbigili – Ismani (Ismani) - Tshs. 1,800,000,000/=. **Jumla: Maji – Tshs. 9,360,986,933/=**
5	**UKIMWI**	• Kupunguza maambukizi mapya ya VVU kutoka 9.1% hadi 0 • Kupunguza unyanyapaa unaosababishwa na ugonjwa wa Ukimwi miongoni mwa watoa huduma, jamii, watumishi na kwa watu wanoishi na virusi vya UKIMWI. • Kupunguza vifo vitokanavyo na UKIMWI	- Kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. - Kuimarisha mfumo wa utunzaji na matibabu (care and treatment) kwa waathirika wa janga la UKIMWI kwa gharama ya Tshs. 460,000,000/= - Kupunguza vifo vitokanavyo na VVU kutoka

		kwa watu wanoishi na maambukizi ya VVU • Kukabiriana na athari zitokanazo na UKIMWI. • Uratibu na usimamizi wa shughuli za mapambano ya dhidi ya UKIMWI katika Halmashauri.	vifo 1,196 mwaka 2016/2017 hadi 0 ifikapo mwaka 2020. - Kupunguza kiwango cha maambukizi ya VVU kutoka 9.1% hadi kufikia 0 ifikapo mwaka 2020. **Jumla: Ukimwi – Tshs. 460,000,000/=**
6	**AFYA**	• Kuimarisha huduma za kinga na tiba • Kuimarisha miundombinu, ujenzi utanuzi na ukarabati wa miundombini wa vituo vya kutolea huduma. • Kuimarisha huduma za rufaa kwa wagonjwa kutoka katika zahanati na vituoa vya afya hadi hospitali ya wilaya na hospitali ya rufaa ya mkoa. • Kuboresha usafi wa mazingira	- Upanuzi wa Kituo cha Afya, Kimande – **Tshs. 100,000,000/=** - Upanuzi wa Zahanati ya Nyang'oro kuwa Kituo cha Afya – **Tshs. 150,000,000/=.** - Ununuzi wa magari 2 "land cruiser hard top" kwa ajili ya ofisi ya DMO na Hospitali ya Tosamaganga @ 160,000,000 – **Tshs. 320,000,000/=** - Ujenzi wa zahanati 10 za vijiji @ 65,000,000 – **Tshs. 650,000,000/=** - Ukarabati wa nyumba za watumishi katika vituo vya afya 3 na zahanati 8 @ 18,820,000 – **Tshs. 207,020,000/=.** - Kuimarisha mfumo wa Utafiti, utunzaji na utumiaji wa takwimu Ofisi ya DMO – **Tshs. 18,000,000/=.** - Kuandaa na kutoa mafunzo kwa kamati 20 za CHF juu ya utendaji na uendeshaji wa mifuko ya CHF ya maeneo yao – **Tshs. 20,000,000/=.** - Ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa vituo vya kutolea huduma 74 wilayani **Jumla: Afya – Tshs. 1,465,020,000/=**
7	**HIFADHI YA MAZINGI-RA**	Kuendelea kudhibiti uharibifu wa mazingira kwa kupanda miti, kuzuia ukataji ovyo wa miti na uchomaji holela wa moto na utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kupanda miti rafiki katika vyanzo vya maji kwa sababu za; - Kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri. - Kuwepo kwa ukataji ovyo wa miti - Kukua kwa mahitaji ya mazao ya misitu (mbao, kuni, mkaa na mijengo). - Uhaba wa maji katika maeneo mengi ya Halmashauri. - Uchomaji moto ovyo miongoni mwa wananchi. - Haja ya kuhifadhi mto Ruaha kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji; na bwawa la Mtera kwa ajili ya kuzalisha umeme na shughuli za uvuvi.	- Kuandaa, kuendesha na kuwezesha utungaji wa sheria ndogo za vijiji 122 - **Tshs. 150,000,000/=.** - Uwezeshaji wa vikosi vya ulinzi wa mipaka ya bwawa la Mtera (BMU) – **Tshs. 17,000,000/=.** - Shughuli za ukaguzi wa maeneo ya hifadhi ya mto Ruaha – **Tshs. 6,000,000/=** - Kupanda miti 200,000 katika shule za Msingi na sekondari - Kuanzisha vikundi 50 vya ufugaji wa nyuki na kuviwezesha kufuga na kuvuna asali. - Kuanzisha vikundi 20 vya kitalii na kuviwezesha kufanya kazi zake. - Kuanzisha vikundi 20 vya USAFI na uboreshaji wa mazingira na kuviwezesha kufanikisha usafi katika miji midogo 5. - Kutambua maeneo manne yanayofaa kwa ajili ya uwekezaji wa kitalii kama hoteli **Jumla: Hifadhi Mazingira – Tshs. 173,000,000/=**

		- Kuyalinda maeneo yaliyo bado na uasili ili yabaki ya asili tofauti na ilivyotokea katika tarafa ya Ismani huko nyuma. - Kuongezeka kwa shughuli za ufyatuaji na uchomaji wa matofali kando kando ya mto Ruaha.	
8	**BARABARA**	• Kuboresha mfumo wa barabara wilayani (District road network) kwa kipindi cha mwaka mzima. - Matengenezo ya barabara ya muda maalumu (Periodic maintenance) - Ukarabati wa barabara (Rehabilitation of roads) - Matengenezo ya sehemu korofi (Spot improvement) - Matengenezo ya kawaida ya barabara (Routine maintenance) - Ujenzi wa madaraja Lengo ikiwa ni kuhakikisha wananchi wana uwezo wa kufikisha mazao yao kwenye Masoko kwa wakati na kuboresha huduma ya mawasiliano wilayani.	- Kuimarisha miundo mbinu ya barabara na madaraja ya barabara za Ifunda – Wasa – Ikungwe; Wasa – Ihomasa – Ulata; Ulete – Lumuli – Itengulinyi; Kalenga – Kiponzelo; Tungamalenga – Mahuninga; Kimande – Kinyika; Kiwere – Igingilanyi; Kisinga – Ilambilole – Mikongwi – Ndolela; Kimande – Makuka – Izazi; Mbuyuni – Mafuruto – Mlowa; Wasa – Makombe – Mahuninga; Kitayawa – Ng'enza – Magulilwa na Ndiwili – Magulilwa - Tshs. **2,840,000,000/=.** - Ununuzi wa mashine ya uchoraji wa ramani (mapping machine) – **Tshs. 5,000,000/=** - Matengenezo ya Tipa la Halmashauri SM 2534 na mitambo kwa ajili ya kutoa huduma za Ujenzi wa miradi ya Maendeleo wilayani.- 30,000,000/= - Uhamasishaji wa jamii zilizo kando ya barabara juu ya Utunzaji na ulinzi wa barabara hizi – **Tshs. 8,000,000/=.** **Jumla: Barabara – Tshs3,270,000,000/=**
9	**UTAWALA** **NA** **UTAWALA BORA**	Utawala bora unaozingatia sharia, taratibu na kanuni za nchi katika maeneo yafuatayo; • Matumuzi mazuri ya rasilimali za nchi. • Maendeleo endelevu • Kupungua kwa umasikini, ujinga na maradhi • Kutokomea kwa rushwa • Huduma bora za jamii • Amani na utulivu • Kuheshimiwa kwa haki za binadamu • Utatuzi wa migogoro kwa mujibu wa sheria na taratibu.	- Uandaaji na utoaji wa mafunzo ya uongozi na uwajibikaji (wajibu wa serikali za vijiji) kwa viongozi wa vijiji 133 – **Tshs. 45,000,000/=.** - Uandaaji na utoaji wa mafunzo ya wajibu wa madiwani katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Halmashauli na Kamati za maendeleo za kata (WDC) – **Tshs. 14,000,000/=.** - Kuandaa na kuendesha mafunzo ya Utunzaji wa vitabu vya fedha, kumbukumbu za mikutano, rejesta za muundo na wakazi na aina ya mifugo kwa watendaji wa serikali za vijiji 133 (maafisa watendaji wa vijiji na wahasibu) – **Tshs. 15,000,000/=** - Ujenzi wa nyumba 5 za watumishi (wakuu wa Idara) @ 50,000,000 – **Tshs. 250,000,000/=.** - Kuwezesha zoezi la Fursa na Vikwazo vya maendeleo (O & OD) na kuandaa taarifa zake kwa kila kijiji – vijiji 133 – **Tshs. 36,600,000/=.** - Uimarishaji wa matumizi ya Mfumo wa PlanRep ndani ya Halmashauri – **Tshs. 20,000,000/=.** - Ukusanyanji, Utunzaji na utumiaji wa takwimu za kisekta na kuhuisha Benki ya takwimu ya Halmashauri – **Tshs. 35,000,000/=**

			- Uratibu, uandaaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa shughuli na miradi ya maendeleo ya Halmashauri kila robo, nusu mwaka na mwaka na kuziwasilisha kwa mamlaka husika kwa wakati – **Tshs. 10,000,000/=.** - Kuwezesha zoezi la uandaaji wa taarifa za miradi ya maendeleo ya Halmashauri ili ziwasilishwe na kukaguliwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa **– LAAC - Tshs. 16,000,000/=** - Kuwezesha uandaaji wa mipango na utekelezaji wa Miradi ya maendeleo vijijini – **Tshs. 45,000,000/=.** - Kujenga na kuimarisha mahusiano kati ya Halmashauri na Sekta Binafsi ili kuharakisha maendeleo - Tshs. 20,000,000/= **Jumla Utawala/Utawala Bora – Tshs. 432,600,000/=**
Jumla Kuu ya Bajeti ya vipaumbele vya Halmashauri kwa mwaka 2017/2018 ni Tshs. 22,954,346,933			

Naomba kuwasilisha:

Robert M. Masunya
Mkurugenzi Mtendaji (W)
IRINGA